## HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA

**MKOA WA GEITA**
SIMU: 028 -2520061
028 -2520003
FAKSI 028 -2520061
Barua Pepe: info@geitadc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S. L. P 139,
**GEITA.**

KUMB.NA. GDC/AF/MAT/V.I/6

09/03/2018

Kwa Wananchi wote,

# YAH: TANGAZO LA KAZI

## (NAFASI ZA AJIRA YA MKATABA KWA KADA ZA AFYA)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ya Afya, Shirika la AGPAHI; anawatangazia wananchi wote wenye sifa kuomba kujaza jumla ya **nafasi 34** za ajira kwa kada za Afya.

### 1.0: AFISA TABIBU (CO) II (TGHS B : TZS. 680,000/=) - NAFASI 11

**1.1: Sifa Mahsusi za Kuajiriwa kwa nafasi hii**

Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo ya utabibu (clinical medicine) ngazi ya stashahada (diploma) katika chuo kinachotambulika na Serikali.

**1.2: Kazi na Majukumu**

1. Kutambua na kutibu wagonjwa wa kawaida
2. Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake
3. Kufanya upasuaji mdogo
4. Kushiriki kupanga na kutekeleza huduma za afya ya msingi
5. Kuelimisha jamii na kutoa ushauri nasaha kwa wagonjwa
6. Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za afya na mfuko wa afya ya jamii
7. Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma
8. Kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za kituo
9. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi



Scanned by CamScanner

## 2.0: AFISA MUUGUZI MSAIDIZI (ANO) II (TGHS B : TZS.680,000/=) – NAFASI 11

### 2.1: Sifa Mahsusi za Kuajiriwa kwa nafasi hii

Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo ya Uuguzi na Ukunga (Nursing and Midwifery training) ngazi ya stashahada (diploma) katika chuo kinachotambulika na Serikali na kusajiliwa (registered) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

### 2.2: Kazi na Majukumu

1. Kutoa huduma za uuguzi na ukunga
2. Kukusanya takwimu muhimu za afya
3. Kuwaelekeza kazi watumishi, wauguzi walio chini yake
4. Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
5. Kutoa huduma za kinga, tiba, afya ya uzazi na motto
6. Kutoa kutoa huduma za wagonjwa majumbani na kutoa ushauri nasaha katika matatizo kwa mtu binafsi au familia husika
7. Kuelekeza na kusimamia mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi
8. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

## 3. 0: MUUGUZI (NURSE) II (TGHS A : TZS. 432,000/=) – NAFASI 11

### 3.1: Sifa Mahsusi za Kuajiriwa kwa nafasi hii

Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo ya Uuguzi na Ukunga (Nursing and Midwifery training) ngazi ya cheti (astashahada) katika chuo kinachotambulika na Serikali na kuandikishwa (enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

### 3.2: Kazi na Majukumu

1. Kufanya kazi za uuguzi na ukunga na kuhudumia wateja katika kituo alichopangiwa
2. Kusimamia na kuratibu kazi za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi
3. Kutoa huduma za wagonjwa na wateja majumbani



Scanned by CamScanner

4. Kutoa huduma za afya-kinga, afya-tiba, afya ya uzazi na mtoto pamoja na huduma rafiki kwa vijana.
5. Kuelimisha wagonja na jamii kuhusu matatizo ya kiafya
6. Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
7. Kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za kituo
8. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzofu na na ujuzi wake

## 4.0: MTEKNOLOJIA MSAIDIZI (MAABARA) (TGHS A: TZS. 432,000/=) – NAFASI 1

### 4.1: Sifa Mahsusi za Kuajiriwa kwa nafasi hii

Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo ya sayansi za maabara za afya (health laboratory sciences) ngazi ya cheti (astashahada) katika chuo kinachotambulika na Serikali.

### 4.2: Kazi na Majukumu

1. Kupima sampuli zinazoletwa maabara
2. Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa maabara za ngazi za juu
3. Kuhifadhi na kufanya ukaguzi wa vitendanishi, vifaa, kemikali katika maabara.
4. Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma
5. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

## 5. 0 : SIFA ZA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

1. Awe ni raia wa Tanzania
2. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na si zaidi ya miaka 45
3. Awe na elimu ya sekondari na cheti cha taaluma cha kidato cha sita na/au kidato cha nne.
4. Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo stahili ya nafasi anayoomba.
5. Awe na uwezo wa kutunza siri za wateja anaowahudumia
6. Awe tayari kufanya kazi na kuishi katika mazingira yoyote hasa vijijini.



Scanned by CamScanner

Ajira hizi ni za mkataba wa miezi sita (6) ambao unaweza kuhuishwa (renewable) baada ya kipindi hicho kwisha. Waombaji watakaoitwa na kufaulu zoezi la usaili watapangiwa kufanya kazi katika Zahanati za Nyarugusu, Lwamgasa, Nyamalimbe, Nkome, Kakubilo na Kasota; na Vituo vya Afya vya Katoro, Nzera, Kashishi, Chikobe na Bukoli. Watumishi wanaofanya kazi kwa kujitolea vituoni watapewa kipaumbele.

**6: JINSI YA KUOMBA**

Andika barua ya maombi kwa mkono ukiambatisha CV na nakala za vyeti vyako vyote vya taaluma na ujuzi. Pia ambatisha picha mbili za hivi karibuni (ppt size).

Barua zote za maombi zitumwe kwa kuwasilishwa mwenyewe mkononi Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Geita au kutumwa kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya ya Geita,

*"AJIRA ZA AFYA"*

S. L. P. 139, GEITA.

au

Kwa njia ya anuani ya barua pepe (email address); **info@geitadc.go.tz**

**7. MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI**

Siku ya mwisho ya kupokea maombi ni Ijumaa tarehe 23 Machi 2018 saa 9: 30 Alasri.

January Bikuba

**K.N.Y: MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**GEITA**



K.n.y. MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
GEITA.

Scanned by CamScanner